



Hifadhi Maji kwa Ajili ya Dharura



Kila mtu



Kila siku

=



Kwa Siku 3

Kila Miezi 6



Mwaga na Ujaze Upya

Usitumie



Kuhifadhia maji



City of Seattle

Seattle
Emergency Management

Ofisi ya Usimamizi wa Matukio ya Dharura Seattle
www.seattle.gov/emergency
206-233-5076

Seattle
Public
Utilities

Hifadhi Maji kwa Ajili ya Dharura

Maafa kama tetemeko la ardhi huweza kuharibu mfumo wa maji. Hifadhi maji ya kutosha kwa angalau siku 3 kwa kila mkazi wa kaya.

Namna ya Kuhifadhi Maji kwa Ajili ya Dharura

Chupa za lita 2 ni bora zaidi kuhifadhia maji, ukifuata maelekezo yafuatayo.

- ★ Hakikisha kwamba chupa ni safi. Weka sabuni kali kiasi cha 1/8 ya kijiko cha chai na vikombe viwili vya maji ndani ya chupa. Funga chupa na kifuniko na utikise taratibu. Hakikisha unasafisha kifuniko na sehemu ya juu ya chupa.
- ★ Mwaga, suuza na jaza maji safi mpaka juu. Funga kizibo vema na andika maelezo kwamba ni maji ya dharura. Andika tarehe ya siku ulipojaza maji katika kibandiko.
- ★ Hifadhi maji kiasi kikubwa uwezavyo! Inashauriwa kuhifadhi chupa sita za lita 2 kwa kila mtu katika familia yako.
- ★ Mwaga na ujaze tena chupa hizo kila miezi 6. (Unapobadili saa majira ya kuchipuka au kupukutika majani ni wakati muafaka wa kumwaga na kujaza maji upya.

ONYO: Usitumie chupa za kioo (zinavunjika kirahisi), majagi ya plastiki (ni vigumu kuyaziba na huvunjika kirahisi) au chupa zilizokuwa na sabuni kali au kemikali za hatari ndani yake.

